

# UKWELI KUHUSU VIJANA NA BANGI.

**Hii hapa habari njema (na ya kushangaza): Tukirejelea taarifa za kuaminika kuhusu bangi na dawa nyingine za kulevyta, vijana huwategemea wazazi wao na watu wengine wazima wanaoaminika maishani mwao.**

Na hizi hapa habari njema zaidi: **Tunajua kwamba kuzungumza na vijana ni jambo linalonufaisha.** Iwe ni kwenye gari, wakati wa chakula cha jioni au matembezi tu mtaani, unapojadili matumizi ya bangi na kijana wako, anasikiliza.

Atakuwa na maswali, na unajua kutohana na uzoefu wako utahitaji kuwa na majibu sahihi.

## Kwa hivyo... bangi inawaathiri vipi vijana?

- 1 Bangi inaweza kuathiri elimu yao. Utumiaji bangi katika miaka ya kwanza unaweza kubadilisha jinsi ubongo wa kijana unavyokua, na pia kuwa na madhara ya kudumu ya kumbukumbu, uwezo wa kujifunza na ustadi wa kiakili.
- 2 Bangi husababisha uraibu zaidi kwa vijana kuliko watu wazima. Katika jimbo la WA, vijana wengi wanaoingia kwenye mipango ya matibabu ya kukabiliana na dawa za kulevyta husema kuwa bangi ndicho kileo kikuu wanachotumia.
- 3 Utumiaji bangi unaweza kuathiri uratibu na muda wa kuchukua hatua, na unahusishwa na ajali mbaya zaidi katika jimbo la WA, hasa bangi inapochanganywa na dawa nyinginezo.
- 4 Utumiaji bangi unaweza kusababisha tabia isiyotabirika, na tabia ya kufanya maamuzi mabaya ambayo yanaweza kumhatarisha mtumiaji na pia watu wengine.
- 5 Ni kinyume cha sheria kwa watu wa umri wa chini ya miaka 21 kutumia bangi. Sheria hii mara nyingi hutekelezwa bila usawa, kwa hivyo kuepuka utumiaji bangi kunaweza kuwalinda vijana dhidi ya kujipata mikononi mwa watekelezaji sheria na mfumo wa sheria za jinai. Kufungwa jela, pamoja na unyanyapaa unaofuatia unaweza kuathiri uwezo wa kupata kazi katika siku zijazo au kupata usaidizi wa kifedha wa chuo kikuu.



Kwa kuwa sasa unafahamu ukweli, **zungumza na kijana wako kuhusu hatari zinazoweza kutokea za utumiaji wa bangi.** Wasiliana kwa uwazi kuhusu sheria na matarajio yako. Mjalishe unajali maslahi yake.

Ili upate maelezo zaidi na kujua zaidi kuhusu ukweli, tembelea **StartTalkingNow.org**. Ikiwa kijana wako angependa kupata maelezo zaidi kuhusu kufanya chaguo bora, anaweza kutembelea **YouCanWA.org**.

Ikiwa kijana wako angependelea zaidi kuzungumza na watu wa rika lake, kuna huduma ya usaidizi ya faragha isiyolipishwa ambayo inatolewa na vijana waliopewa mafunzo. Mhimize kijana wako kupiga simu, kutuma SMS au kupiga gumzo kwenye **1-866-TEENLINK (833-6546)**.

Ikiwa unaamini kwamba kijana wako anatatizika kuacha bangi au dawa nyinginezo za kulevyta, wasiliana na daktari wake au upige simu **Washington Recovery Help Line** kuitia **1-866-789-1511**.